



Wizara ya Afya Zanzibar

Fomu ya Makubaliano ya Kupeana Data

Mkataba huu unaweka Kanuni na masharti ambayo Taasisi/Shirika/Watu binafsi ("Mtumiaji Data") wanaweza kutumia data za Wizara ya Afya Zanzibar. Kama ifuatavyo:

1. Data zilizohamishwa kwa Mtumiaji wa Data chini ya masharti ya Makubaliano haya zitatumika kwa madhumuni yaliyotajwa katika Fomu ya Maombi ya Data iliyoidhinishwa.
2. Kwa wale tu waliotajwa katika Fomu ya maombi iliyoidhinishwa ndio ambao watatumia data. Mtumiaji wa Data lazima aijulisha Wizara ya Afya, kwa maandishi, ikiwa watu wa ziada wanahitaji kutumia data kabla ya watu hao hawajapewa data hizo.
3. Mtumiaji wa Data hatoruhusiwa kutoa data kwa watu wengine kabla ya kupata ithibati ya maandishi kutoka Wizara ya afya.
4. Data zilizotolewa kwa watu wengine na mtumiaji zitabaki kuwa ni mali ya Wizara ya Afya na zitarudishwa Wizara ya Afya au kuharibiwa baada ya kuvunjwa kwa mkataba wa makubaliano mpaka kuwe na makubaliano ya kabla ya kimaandishi kutoka Wizara ya Afya.
5. Mtumiaji wa Data hatotakiwa kutoa taarifa ya mtu iliyomo katika seti ya data anayoifanyia kazi.
6. Mtumiaji wa Data hatoruhusiwa kutoa taarifa yoyote inayohusina na mtu, kwa njia ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja.
7. Mtumiaji wa Data atatoa data kutoka kwa mtu mwingine, kuchapisha, au kutoa matokeo au mapendekezo yanayotokana na data baada ya kupata idhini ya maandishi kutoka Wizara ya Afya.
8. Mtumiaji wa Data akubali kufuata hatua zote muhimu za kulinda usalama na uadilifu wa data. Mtumiaji wa Data atapaswa kuijulisha Wizara ya Afya maramoja ikiwa data zitatumwa vibaya.
9. Mtumiaji wa Data atapaswa kutoa taarifa za mabadiliko mapya kwa Wizara ya Afya pale anapohitajika kufanya hivyo.
10. Mtumiaji wa Data atapaswa kutoa maelezo ya kina ya data iliyoombwa, ikijumuisha muundo wake, maudhui, na data zinazotoa maelezo ya taarifa nyengine husika (JSON, XML, CSV, n.k).
11. Mtumiaji wa Data atapaswa kukubali kanuni na masharti ya Mkataba wa kupeana data kabla ya data yoyote kutolewa kwake.

Kwa makubalianano ya pande zote mbili, wawakilishi walioidhinishwa kupeana Data watalazimika kusaini makubaliano kufikia tarehe ya mwisho iliyotajwa hapo chini.



MTUMIAJI WA DATA

JINA [TAASISI]:
ANUANI [TAASISI]:
MAWASILIANO YA MTUMIAJI:
USHIRIKIANO:
BARUA PEPE:
SIMU:
SAINI:
TAREHE:.....

WIZARA YA AFYA ZANZIBAR

JINA:
CHEO:
SAINI:
TAREHE: